Mwongozo Wa Mwalimu

5

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

## Kuonekana mwenye mafanikio machoni pa Mungu



MVMM

Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

## Kuonekana mwenye mafanikio machoni pa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

## Kuonekana mwenye mafanikio machoni pa Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la tano

Maandiko yanayotumiwa katika kitabu hiki yametoka kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kupatianwa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bila malipo. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Successful Christian Living, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, mashuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 08-2023

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

Dhamira kuu ya kozi hii ni kuonyesha jinsi Wakristo wanaweza kuishi kwa mafanikio kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Kozi hii inachanganua mambo tofauti yanayoweza kumfanya mtu ashuhudie kukua kwa kweli kama Mkristo.

1

### Sura ya 1. Mimi ni nani?

Sura hii inadadavua jinsi Mungu alituumba na anachofikiria kutuhusu. Tunajifunza pia jinsi mili yetu, hulka na nyoyo zetu hubadilika tunapokuwa Wakristo. Maangazio maalum huelekezwa kwa fahamu zetu, na wajibu wake katika ukuaji wa kila Mkristo mpya.

2

### Sura ya 2. Hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa

Hatua tano za kujadiliwa ni:

1. Kuwa Mkristo
2. Badilisha jinsi unavyofikiria.
3. Weka malengo mapya
4. Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako
5. Wafahamishe wengine kile Kristo amefanya katika maisha yako

3

### Sura ya 3. Roho Mtakatifu

Sura hii katika kozi inajadili Roho Mtakatifu ni nani na jinsi gani anavyoweza kutusaidia kuishi maisha ya Mkristo mwenye mafanikio.

## Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa ulio na jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo
2. Mwongozo Wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo kuhusu jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

# Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani, ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

## Jinsi ya kutumia Mwongozo huu Wa Mwalimu

### 1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa ufupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilika, na wakati kila chemsha bongo na mtihani zitatolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala ambayo haijaandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwa Mwongozo wa Mwanafunzi au kwa Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika "Kufanyia Kazi Somo Maishani." Umuhimu wa kipengele hiki haueelezeki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba unatoa nafasi ya kutosha ya kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo, kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikidumu kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihani. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi

minne, kama darasa litakutana kwa siku tano kwa wiki. Ikiwa darasa ni la saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa mwaka mmoja hivi. Mengi ya masomo haya yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

## 2. Mwongozo Wa Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwanafunzi kinaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika ili kujiandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili iwe kama marudio na kama njia ya kusisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie kumbukumbu darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani yatawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

## 3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwaasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

## 4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

## 5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa ***Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***.

# Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Taasisi Ya Kanuni Za Maisha (Institute in Life Principles) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Taasisi Ya Kanuni Za Maisha (Institue in Life Principles).

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wapya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya.
Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

# Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kupatianwa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali fulani, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kwenye mtandao kwa tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bila malipo. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty

# Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vyuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mtazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Matendo Ya Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, ***Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha masomo hayo.

# Mipangilio ya Masomo

# Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo.

# Maelezo ya jumla ya kozi

1. Siku moja au mbili kabla ya kikao cha kwanza darasani, unaweza kuwapa wanafunzi utangulizi wa kozi hii na kuwapa kazi ya kwanza. Ikiwezekana wape mwongozo kabla ya kuanza kufunza kozi hii.

2. Punde baada ya mukhtasari huu, (ukurasa wa 11) uwe na nakala ya *Orodha ya kazi za darasani*, ambayo inatoa makataa ya kumaliza kila kazi ya darasani. Uwape wanafunzi wajaze tarehe mwafaka wakitumia nakala tupu za *Orodha ya kazi za darasani* iliyoko nyuma ya mwongozo wao.

3. Wajulishe wanafunzi ya kwamba wanastahili kuwa na Mwongozo wa somo Zoezi 1, *"Dhamiri Yangu,"* kamili wakija kwa darasa la kwanza.

4. Mwongozo wa mwanafunzi unanweza kutwaliwa kwao wanafunzi wakati wa kutangulizwa kwa kozi na pia kuandamana na Mwongozo wa somo. Waelekeze wanafunzi wasome sura ya kwanza na ya pili – Hatua ya kwanza na ya pili kwa matayarisho ya kikao cha darasa la kwanza.

5. Unakisia kuwa na vikao vingapi vya darasa kufunza kozi hii? Kuna mipangilio ya masomo kwa vikao vinne vya darasa katika kurasa zifuatazo. Hata hivyo, kozi hii inaweza kupanuliwa ikajumlisha vikao vya ziada. Kwa mfano, mpangilio wa kwanza unaangazia sehemu kuu ya kwanza yenye mada *"Mimi ni nani?"* na hatua mbili za kwanza za *"Hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa."* Ungetaka kutumia kikao cha kwanza kufanya Sura ya kwanza, *"Mimi ni nani?"* Pia unaweza kutumia kikao kizima kwa kila mojawapo ya zile hatua 5 za kuwa Mkristo mwenye mafanikio ambazo zinaangaziwa katika sura ya Pili kwa Mwongozo wa mwanafunzi.

   Sura ya 3 ya kozi hii inazungumzia Roho Mtakatifu. Sura hii imeangaziwa katika mpangilio wa nne kwa mwongozo wa walimu. Hata hivyo, ukipenda kutumia muda Zaidi kwa mswada huu, unaweza kuzinyambua hoja zikawa mbili, tatu au hata nne.

6. Iwapo utaifunza kozi hii kwa vikao vinne, basi utapaswa kutathmini sehemu utakazopitia kwa haraka, na zile zitakazoangaziwa kimsingi katika kila kikao cha darasani. Maswala kadhaa katika kozi hii yameangaziwa kwa kina kirefu katika kozi za *Mafunzo ya vikundi kwa Maisha Mapya*, hususan *Mitazamo, Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo? Nguvu Za Kiroho, Na Mambo Yasiyo Ya Kawaida* na *Jinsi ya kujifunza Biblia.*

7. Wakristo wengine wako na wakati mgumu kupata usawaziko kati ya jitihada za kibinadamu na nafasi ya Mungu ya kuwa Mkristo mwenye mafanikio. Inatupasa kusisitiza kote kote katika kozi hii, jukumu kuu la Mungu kwa kutusaidia kukua kiroho.

8. Ubatizo kwa Roho Mtakatifu ni mada inayoweza kuleta ukinzani baina ya madhehebu mengine. Kurasa kadhaa katika Mwongozo wa mwanafunzi zinajadili kipaji hiki. Iwapo dhehebu lako linashikilia msimamo ulio tofauti sana na ule uliopo katika kitabu hiki, basi itakupasa kuamua jinsi ya kutumia kozi hii katika kanisa lako. Iwapo uko na tatizo na jinsi mada hii imechanganuliwa katika Mwongozo wa mwanafunzi, tafadhali wasiliana na mchapishaji, *Changa moto kwa Vijana*, kwa kutumia anwani ilioko katika ukurasa wa dibaji.

# Orodha ya Kazi za Darasani

**Jina La Somo** Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

| **Chemsha Bongo** | Maandiko Ya Kukariri | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 | 1 Wakorintho 10:29 | Somo La 3 |
| 2 | Yohana 16:13 | Somo La 4 |
| 3 | | |

| **Zoezi** | Jina La Kazi | Tarehe ya Kuwasilisha |
|---|---|---|
| 1 | Dhamiri Yangu | Siku Ya 1 |
| 2 | Malengo katika Biblia | Siku Ya 2 |
| 3 | Kuweka Malengo katika Matendo | Siku Ya 3 au 4 |
| 4 | Hisia Zangu | Siku Ya 3 |
| 5 | Roho Mtakatifu ni nani? | Siku Ya 4 |
| 6 | Roho Mtakatifu Maishani Mwangu | Siku Ya 4 |

**Mtihani** Tarehe Siku Ya 5

1

# Somo la 1
# Mimi ni nani?

**1. Kweli Kuu ya Kibblia**

Ninapaswa kumsikiliza Mungu anaponizungumzia kupitia ufahamu wangu.

**2. Mstari Mkuu: Methali 20:27**

Ufahamu wa mwanadamu ndio kurunzi ya Bwana inayofichua nia iliyofichwa.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya Kwanza na ukurasa 11-14 katika Sura ya Pili kwa Mwongozo wa Mwanafunzi zinaambatana na somo hili. Mwongozo wa Somo Zoezi 1, *"Dhamiri Yangu"* pia inatangamana na somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo: "Mafanikio ni nini?" (Dakika 5-10)**

Chagua mojawapo ya matendo yafuatayo kutanguliza somo.

**Chaguo A. Ni upi mtazamo wako wa mafanikio?**

Chukua dakika chache kujadili maswali haya:

1. Ulimwengu hupimaje fanaka?
2. Ni katika sehemu zipi za maisha yako ambapo ulimwengu unakuchukulia kuwa na mafanikio?
3. Mitazamo yako ya fanaka inawiana au kutofautiana vipi na ile ya wenzako wasio Wakristo?
4. Mitazamo yako ya fanaka ya ukweli imegeuka vipi kwa miaka mitano iliyopita?

**Chaguo B. Ulimwengu huchukulia vipi fanaka?**

Waelekeze wanafunzi wako wapitie majarida na kukata picha zinaonyesha mtazamo wa dunia wa fanaka. Waelekeze basi wazibandike zile picha kwa karatasi kubwa kubwa na kuziangika ukutani kwa sababu ya somo hili. Katika kozi hii, utarejelea mara kwa mara picha hizi ukionyesha jinsi Mungu aonavyo fanaka.

**5. Mukhtasari wa somo**

Chukua yamkini nusu ya muda uliotengwa kwa kikao hiki kuangazia *“Mimi ni nani?”* Sura ya 1 katika Mwongozo wa mwanafunzi. Mojawapo ya hatua msingi sana katika kukua kiroho ni kuwa na mtazamo wa Kibiblia kwa nafsi yako mwenyewe. Swala hili limengaziwa kwa kina katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya, Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe.*

Wanafunzi wanapaswa kuwa na ufahamu mzuri wa sehemu za mtu za kimwili, kimawazo na hata kiroho. Kwa kutumia mawazo haya, wataweza kuelewa jinsi kila sehemu ihusikavyo kwa kuwa Mkristo mwenye mafanikio.

Awamu ya pili ya kikao cha darasa la leo inagusia kwa ufupi hatua mbili za kwanza za kuwa Mkristo mwenye mafanikio. Hatua ya kwanza ni *“Kuwa Mkristo”* na ya pili ni *“Badilisha jinsi unavyofikiria.”*

Muda utakaochukua kwa maswala haya matatu utategemea ukomavu wa kiroho wa wanafunzi wako.

**6. Jadili Hoja A, “Kile Mungu anasema kunihusu”**
**(Dakika 5-10   Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5-6)**

Zipitie zile hoja saba zilizoorodheshwa katika ukurasa 5-6 kwenye Mwongozo wa mwanafunzi, zinazoeleza anachosema Mungu juu yetu. Wanafunzi watafute na kusoma maandiko tofauti yaliyoorodheshwa katika kila hoja.

**7. Tanguliza vile viungo vitatu vya mtu**
**(Dakika 3-5   Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 7)**

Sehemu ifuatayo ya somo inaangazia viungo vitatu vya mtu – vya kimwili, kimawazo na kiroho. Unapotanguliza maelezo haya, eleza kwamba Biblia inawasilisha mtazamo kwamba sisi ni viumbe kamili. Maangazio yetu ya viungo hivi vitatu ni kwa minajili ya kutufanya tuelewe vyema jinsi Mungu alivyotuumba.

Hizi sio fafanuzi kamilifu za viungo vitatu vya mtu. Vile vile, taswira inayoelezewa ya mtu sio sura kamili ya binadamu. Zote hizi – mwili, mawazo na roho zinahusiana kwa karibu, ilhali zenye tofauti za kipekee. Zote tatu zimo ndani mwako. Mungu alikuumba kwa njia ya pekee tofauti na mtu awaye yeyote.

1

## Mimi ni nani?



**B. Niko na mwili halisi**

1. Fahamu tano
   Fahamu ya nuru (Kuona)
   Fahamu ya sauti (Kusikia)
   Fahamu ya harufu (Kunusa)
   Fahamu ya ladha (Kuonja)
   Fahamu ya mguso (Mguso)
2. Vichocheo vya kimwili
   Maji
   Chakula
   Hewa

**C. Niko na utu**

(Vipengele vya kisaikolojia)

1. Mawazo yangu
2. Hisia zangu
3. Maamuzi yangu
4. Dhamiri yangu

**D. Niko na roho**

Mahali ambapo anaishi
Warumi 8:9

Jaribu kuepuka mjadala wa neno, "nafsi". Eleza ya kwamba maneno haya "haiba" na "saikolojia" hayakuwa yamevumbuliwa hadi karne chache zilizopita. Maneno haya hayakutumika wakati wa kuandika Biblia. Maandiko hayarejelei viungo tofauti vya haiba. – Mafikira yetu, hisia, nia na ufahamu.

**8. Jadili Hoja B. "Niko na mwili halisi"**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 7-8)**

Kwa haraka pitia hoja B, "Niko na mwili halisi". Tazama ukurasa 7-8 katika Mwongozo wa mwanafunzi kwa taarifa zaidi kuhusu hoja hii. Ungetaka pia kugusia kwa mpito, vichocheo vya kimwili ambavyo Mungu amewaumbia watu. Mwongozo wa mwanafunzi haujadili swala hili kwa kina. Mahitaji yetu ya chakula, hewa na makao yanahusiana moja kwa moja na miili yetu halisi.

Taja kwa kifupi kwamba tunahitaji kutunza mili ambayo tumepewa na Mungu. Lishe bora na mazoezi ni mambo mawili haswa yaliyo na athari kuu jinsi mili yetu hufanya kazi.

**9. Tambulisha Hoja C, "Niko na utu"**
**(Dakika 1-2 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8-10)**

Nyenzo za ukurasa 8-10 katika Mwongozo wa mwanafunzi zinaangazia vipengele vinne tofauti vya haiba – Mafikira, hisia, maamuzi (nia), na ufahamu. Hakikisha kwamba wanafunzi wako wanaelewa tofauti kati ya vitu hivi vinne vyenye ushawishi

mkuu kwa haiba yao. Biblia ina mengi ya kusema kuhusu kila mojawapo ya vipengele hivi vinne vya mwanadamu.

Sehemu hii tungeipa kichwa "kipengele cha kisaikolojia cha mwanadamu." Lakini, baadhi ya wanafunzi wako huenda wakawa hawana ufahamu wa dhana za msingi za saikolojia, na kwa hivyo tukachagua kichwa "Niko na haiba." Tunatumia neno "haiba" kwa ujumla, wala sio kwa maana batini ya kisaikolojia.

**10. Jadili Hoja C-1, "Mawazo yangu"**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8)**

Eleza tofauti kati ya ubongo na fikira. Ubongo wako ni kiungo cha mwili. Fikira yako huundwa na kuhifadhiwa kwenye ubongo wako. Huu ni mfano mwafaka wa uhusiano kati ya sehemu ya kimwili na ile ya kisaikolojia ya mwanadamu. Maudhui haya ya mafikira yameangaziwa kwa undani katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* yenye mada, *Mitazamo.*

**11. Jadili Hoja C-2, "Hisia zangu"**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8)**

Pitia hoja hii kwa upesi kwa sababu tutaliangazia eneo hili kwa kina tutakapokuwa tunajadili hatua ya nne ya jinsi ya kuwa mkristo mwenye mafanikio, *"Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako."* Fafanua ya kwamba hisia zetu ni kipengee kimoja cha haiba yetu. Lakini hisia zetu haziwezi kuguzwa kwa mikono. Hauwezi kujikata ukaona hasira na hofu kwa macho. Hisia zetu ni za asili hata ingawaje haziwezi kuguzwa kwa mikono. Mungu alituumba kwa hisia hizi na anataka tuzitumie daima kwa ukomavu.

**12. Jadili Hoja C-3, "*Maamuzi yangu*"**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8)**

Sisi hufanya maamuzi na nia zetu. Kipengele hiki cha haiba tulikipata pale Mungu alipotuumba. Maaamuzi tunayoyafanya, na jinsi tunavyoyafanya hututofautisha na kutufanya kila moja kuwa spesheli. Tutaliangazia jambo hili kwa kina katika somo 2 tutakapokuwa tunajadili hatua ya tatu ya kuwa Mkristo mwenye mafanikio, *«Weka malengo mapya».*

**13. Jadili Hoja C-4, "*Dhamiri yangu*"**
**(Dakika 10-20 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10)**

Chukua muda wa kutosha katika mada hii kujadili maana ya ufahamu na jinsi unavyoathiri haiba. Tumia matendo katika Mwongozo wa somo Zoezi 1, *"Dhamiri yangu,"* unapopitia hoja hii. Maswali tofauti yanatoa mtazamo pana wa mada hii.

Hakikisha unajadili msawaziko tunaouhitaji kuhusu ufahamu wetu. Ufahamu wetu ni mwongozo tuanaoweza kuusikiliza tunapojaribu kufanya anachostahili Mungu, tufanye. Hata hivyo, wengine huchananyikiwa wanapojaribu kusikiliza ufauhamu wao. Wao hupata ugumu kutofautisha msimamo wa kikweli wa Roho Mtakatifu na mafikira mengine yanayowajia moyoni.

Tilia mkazo umuhimu wa kutumia mijarabu mingine kubaini kama Mungu anatuzungumzia kupitia ufahamu wetu, au kama fikira hilo linatujia toka pengine tofauti. Majiribio mengine mawili yanaweza kutumika – Biblia na ithibati ya Wakristo wengine wakomavu.

Eleza jinsi ufahamu wako hutumika kukujulisha kwamba uko sawa au umekosa katika kutekeleza mambo fulani. Waeleze wanafunzi wako jinsi Mungu anakuzungumzia kupitia ufahamu wako. Washirikishie vidokezo ulivyong'amua kuhusu jinsi ya kuwa makini kwa ufahamu wako.

Kosa jingine ambalo hutenda baadhi ya Wakristu ni kudhania ya kwamba ufahamu wao utawajulisha kama wako sawa au la wakati wote. "Lazima iwe sawa kwangu mimi kunywa pombe na kuvuta sigara, kwa sababu nifanyapo hivyo, sina dhamiri yenye hatia". Hatuna hakikisho ya kwamba Mungu atatuzungumzia siku zote kupitia fahamu zetu. Ama njia mwafaka ni kusema "Unaweza ukakosa kumsikia Mungu akikuzungumzia kwa sababu ya kutotilia maanani ufahamu wako."

Katika mambo mengi ya kutiliwa shaka, Biblia inatufasiria dhambi ni nini. Mtu anapokiuka amri moja ya Mungu, anaweza kupata hukumu kali au pia akakosa kuhukumiwa kabisa. Mungu humtendea kila moja wetu kwa njia ya kipekee. Katika Zaburi 51, Daudi anasema wazi kwamba alikuwa hukumuni kwa sababu ya kutotubu dhambi zake.

Mfalme Daudi alijua jinsi ya kusikiliza ufahamu wake. Kama mtu husema hana dhamiri ya hatia kuhusu jambo lolote, basi tatizo huenda likawa kwamba mtu huyu hatilii maanani ufahamu wake. Jinsi waumini wakuavyo karibu katika uhusiano wao na Mungu, ndivyo wanatazamiwa kuwa makini zaidi kubaini anapowazungumzia Mungu kupitia ufahamu wao.

**14. Jadili swala la "Je, vipi kuhusu hatia ya uwongo?
(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10)**

Wengi wa Wakristo wapya hukumbana na changamoto ya kujaribu kubaini tofauti kati ya hatia halisi na hatia ya uwongo. Unapoangazia hoja hii, wahimize wanafunzi wako kuwa wanyoofu na Mungu. Wasaidie kuona umuhimu wa kutumia neno la Mungu kama njia halisi, wala sio hisia.

Shetani huweza kuleta hisia za hatia ya uowngo – ambazo unaweza kuhisi sawia na hatia halisi – kujaribu kututia hukumuni na katika hali ya kuchanganyikiwa.

Tumia 2 Wakorintho 10:3-5 kusisitiza umuhimu wa kujua jinsi ya kunasa kila fikira na kulifanya kumtii Kristu. Ni lazima wajue jinsi ya kutumia Biblia kama chimbuko la kweli kuchunguza hisia zao na kutathmini kama zinatoka kwa Mungu ama mahali pengine tofauti.

**15. Jadili Hoja D, “Niko na roho”**
**(Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 10)**

Swala hili huenda likawa gumu au rahisi kwa wanafunzi wako kupata, kulingana na malezi yao ya kidini au umri. Epuka majadiliano ya kina ya kitheolojia kuhusu, roho, nafsi na mwili na mahusiano yao.

Wazo kuu tunalotaka kuliangazia hapa ni kwamba, Mungu huja na kukaa ndani ya nyoyo zetu tunapokuwa Wakristo. Nyoyo zetu zitaishi milele, lakini mili yetu itakufa.

**16. Hitimisho la Sura ya 1, “Mimi ni nani’’ (Dakika 3-5)**

Mungu alitenda maajabu kwa kutuumba. Kila mmoja wetu ni wa kipekee kwa Mungu. Kama wanafunzi wako wanajielewa na kujua jinis Mungu alivyowaumba, basi wanapaswa kufanya vyema zaidi katika maeneo ambayo wako na matatizo. Pindi wajuapo tatizo, basi wanahitajika kutia bidii kupata suluhu.

**17. Tambulisha Sura ya 2, “Hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa”**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11)**

Kwa ufupi tanguliza Sura ya 2, “Hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa.” Pitia hoja kuu katika maelezo ya utangulizi kwenye ukurasa 11 – Mwongozo wa mwanafunzi. Jambo kuu la kuwasilisha ni kwamba sio hizi hatua tano pekee zistahilizo kutekelezwa ili kuwa mwenye mafanikio, kwa mtazamo wa Mungu. Hizi tu ni za msingi. Inaweza kumchukua mtu majuma, miezi, miaka na hata maisha yote kubobea katika hatua hizi tano. Haijalishi ni muda upi utakawia; mchakato huu huanza kwa hatua ndogo ndogo, siku baada ya nyingine.

Unaweza kuchukua dakika chache kujadili tofauti kati ya mtazamo wa Mungu wa mafanikio na ule wa ulimwengu. Labda jina jingine la kozi hii lingekuwa “Maisha ya Kiimani ya Mkristo.” Hii inatokeza moja katika ya vipengele vya fanaka katika mtazamo wa Mungu.

**18. Jadili Hatua ya 1, “Kuwa Mkristo”**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 12-13)**

Iwapo darasa lako liko na wanafanzi kadhaa ambao si Wakristu, basi itakuwa vyema ukiwa mwangalifu sana kwa muda unaoutumia kujadili hoja hii. Kama uko na uhakika kwamba wanafunzi wako wote ni Wakristo, basi unaweza kupitia hatuia hii kwa haraka.

Rejelea Mwongozo wa mwanafunzi ukurasa wa 12-13 kwa maelezo zaidi ya swala la kujadili. Onyesha jinsi kila sehemu ya haiba inahusika katika kuwa Mkristo. Mwongozo wa mwanafunzi hautaji wajibu wa ufahamu, lakini unaweza kuambatanisha hoja hilo kwa urahisi utakapoangazia hoja ndogo a, *“Mwache Mungu akuzungumzie kupitia Biblia.”*

Kwa ufupi tena eleza kwamba mtu anapokuwa Mkristo, Mungu huja na kukaa ndani ya mtu huyo. Huleta maisha mapya kwa roho iliyokufa. Wakumbushe kwamba mtu anapokuwa Mkristo, Mungu humgeuza roho mara moja.

Sehemu nyingine za mtu huyo – Mwili halisi na haiba (mawazo, hisia, nia na fahamu) hazigeuzwi papo hapo wakati wa wokovu. Mungu anataka kugeuza sehemu hizi ndani yetu, lakini ni lazima tushirikiane naye kupata kukua katika sehemu hizi nyingine.

Hatua ya kwanza ya kuwa Mkristo mwenye mafanikio huweza kulinganishwa na kuzaliwa kwa mwana. Baada ya kuzaliwa, hatua mpya katika maisha huanza.
Ukuaji ni muhimu ikiwa mwana atatarajiwa kuhitimu ukomavu. Ndivyo hivyo pia kwa kuzaliwa na kukua kiroho.

**19. Jadili Hatua ya 2, "Badilisha jinsi unavyofikiria"**
**(Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13-14)**

Ikiwa uko na muda, kwa kifupi jadili hatua ya 2, *"Badilisha jinsi unavyofikiria."* Chukua muda kusoma na kujadili Warumi 12:2 inayozungumzia umuhimu wa kurotubisha mawazo yetu. Waambie wanafunzi wako kwamba mada hii inashughulikwa kwa undani katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya – Mitazamo* na *Majaribio.*

**20. Matumizi binafsi (Dakika 5-10)**

Angazia matumizi binafsi ya ukweli halisi ya Kibiblia, "Ninapaswa kumsikiliza Mungu anaponizungumzia kupitia ufahamu wangu." Jadili njia wanazoweza kuwa makini zaidi kwa Roho Mtakatifu.

**21. Kazi ya ziada**

A. Sahihisha *Mwongozo wa somo Zoezi la 1, "Dhamiri yangu,"* mwishoni mwa kikao cha darasa.

B. Waelekeze wanafunzi kusoma sura ya 2 katika Mwongozo wa Mwanafunzi wakijitayarisha kwa kipindi kinachofuata.

**22. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 2
# Hatua ya 3: Weka malengo mapya

2

**1. Kweli Kuu ya Kibiblia**

Katika mafunzo yangu ya Biblia ya kila siku, inanipasa kuweka malengo ya kutumia ninapokumbana na changamoto.

**2. Mstari Mkuu: Zaburi 16:9 Toleo la Swahili Union**

Tunapaswa kufanya mpango – tukimtegemea Mungu kutuelekeza.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Ukurasa 11-19 katika Mwongozo wa Mwanafunzi na Mwongozo wa somo Zoezi 2 na 3 zinaambatana na somo hili. Zoezi 2, *"Malengo katika Biblia"* inapaswa kukamilishwa kabla ya kikao cha darasa hili kuanza. Zoezi 3, *"Kuweka Malengo katika Matendo"* ni kazi ya ziada ambayo haipaswi kuanza hadi somo hili litakapokuwa limefunzwa.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5)**

**Chaguo A. Maazimio ya Mwaka Mpya**

Anza somo kwa majadiliano ya maazimio ya Mwaka Mpya.

a. Je, wewe hufanya maazimio ya mwaka mpya?

b. Je, umefanikiwa kuyatimiza maazimio haya hapo awali?

c. Ikiwa huwa haufanyi maazimio ya Mwaka mpya, kwa nini?

d. Ni ipi mifano ya malengo makuu ambayo tayari umetimiza maishani mwako?

e. Je, una malengo ya maisha yako ambayo bado haujayatimiza?

**Chaguo B. Mchoro wa wasifu wa John Goddard**

Toa muhtasari mfupi wa maisha ya John Goddard. Dondoo hili linapatikana katika nakala ya jarida la *Reader's Digest* ya Oktoba, mwaka 1983, ukurasa wa 128-132. Kichwa cha dondoo ni *"I Wanted to Do It All."* Goddard aliandika orodha ya malengo 127 ya maisha yake alipokuwa na miaka 15. Kwa mukhtasari, eleza yaliyojiri katika kuyatimiza malengo haya. Kufikia miaka 59 Goddard alikuwa ameyatimiza malengo 106 kwa malengo yale yote 127 kwa jumla.

Tumia hadithi hii kushuhudia kwamba malengo yanaweza kuyapa mwelekeo maisha yako. Unaweza kuyapitia maisha na kutimiza machache, au kuweka malengo binafsi na kudiriki mengi zaidi. Unaweza kumuuliza mwanafunzi moja katika darasa asome hadithi hii awali na kutoa ripoti kwa darasa zima.

**Chaguo C. "Laiti ningalikuwa na…"**

Anza somo kwa kuwapa wanafunzi sentensi zifuatazo wakamilishe. Umpe kila mwanafunzi nakala ya sentensi. Au uziweke sentensi paruwanja kwa ubao. Uwagawanye wanafunzi kwa vikundi vya watu 3-4. Kisha uwaambie wakamilishe sentensi hizo zote. Watakapomaliza, wakubalie kuonyeshana majibu.

**Sentensi za kukamilishwa.**

1. Kama ungesafiri popote duniani, ungechagua kwenda ……… ?
2. Kama ungechagua kazi yoyote, ungekuwa ………?
3. Kama ungepata udhamini kamili wa kujiunga na shule au chuo chochote kile humu nchini, ungependa kusoma (somo lipi) ………. katika …………. (shule/chuo gani)
4. Kama ningekuwa na dola milioni moja, ningezitumia kwa …………….

**5. Marejeleo ya somo la Kwanza (Dakika 2-3)**

Chukua dakika chache mwanzoni mwa somo kufanya marejeleo ya **"Hatua tano za kuwa Mkristo aliyefanikiwa"** ulizopitia katika somo la kwanza.

Hatua ya 1, Kuwa Mkristo

Hatua ya 2, Badilisha jinsi unavyofikiria

**6. Hatua ya 2, "Badilisha jinsi unavyofikiria"**
**(Dakika 5-10 Mwongozo Mwanafunzi, ukurasa wa 13-14)**

Iwapo haukujadili hatua ya 2, *"Badilisha jinsi unavyofikiria"* katika somo lililopita, basi kwa ufupi pitia leo. Eleza kwamba tutapitia mada hii kwa undani katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya, Mitazamo* na *Majaribio.*

**7. Tambulisha hatua ya 3, "Weka malengo mapya"**
**(Dakika 5, Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 14-19)**

Kama haukutumia Chaguo C katika "Zoezi la utangulizi wa somo" mwanzoni mwa somo hili, basi waulize wanafunzi walitafakari swali hili. "Kama ungekuwa chochote utakacho katika maisha, ungependa kufanya nini/kuwa nini/kuwa na nini? Waruhusu waangaliane na kujadili majibu yao.

Angazia mahusiano ya karibu baina ya ndoto na malengo. Kuweka shabaha ndiyo njia kamili ya kutimiza ndoto zetu. Somo letu leo litaangazia jinsi tunaweza kuleta nia zetu kunyenyekea mbele ya Mungu. Ni lazima tuweke malengo na matamanio yetu chini ya uongozi wa Mungu na tufanye mambo anayotuamuru Mungu tufanye. Pia tutajadili njia ya kufanya maamuzi yenye utiifu kwa Mungu.

**8. Vielezi**

Tumia vielezi maradufu katika somo hili. Usipofanya hivyo, wanafunzi wengi hawataelewa mambo ya kimsingi utakayojaribu kuwafunza. Vielezi kutokana na matukio halisi ya maisha ya kila siku vitahakikisha kwamba hili halitakuwa tu somo la nadharia. Fanya iwe halisi!

**9. Fasili malengo (Dakika 3-5)**

Utafasili kwanza neno, “malengo,” na utoe mifano ya yale tunayoyazungumzia leo. Linganisha hili na matendo uliyoyatumia kuanzisha somo. Dhamira ya somo hili ni kuangalia aina tofauti ya maamuzi tunayoyafanya maishani mwetu.



**10. Je, Mungu ananitaka mimi niwe na maazimio ? (Dakika 5-10)**

Wakristu wengine wanaaminia kusudi la kumkubalia Roho Mtakatifu atuongoze katika kila fani ya maisha yetu. Hawataki kuingilia ya Mungu na hivyo kukosa kufanya mapenzi yake. Wanahofia kwamba kuweka malengo binafsi kunaashiria kwamba hawamuamini Mungu kuelekeza maisha yetu. Sisitiza haja ya kuwa na usawaziko. Kisha angazia maswali 1-5 katika Mwongozo wa Somo, Zoezi 2, «Malengo katika Bibilia». Tumia maandiko haya kufafanua jinsi Mungu anatutaka kuweka malengo tunapotaka kuwa Wakristu wakomavu.

**Kutoka kwa Mwongozo wa somo, Zoezi 2, “Malengo katika Biblia”**

Swali la 1: Elezea kwa maneno yako mwenyewe mistari hiyo inasema nini kuhusu sehemu yako na sehemu ya Mungu katika kuweka na kukamilisha malengo.

**Mithali 16:1** (Toleo la Swahili Union)

Tunaweza kufanya mipango lakini matokeo yako mikononi mwa Mungu.

**Mithali 16:9** (Toleo la Swahili Union)

Tunapaswa kufanya mpango – tukimtegemea Mungu kutuelekeza.

Sehemu ya Mungu: ________________________________________

Sehemu wangu: ____________________________________________

Swali la 2: Mungu anatupatia hadi gani katika Wafilipi 4:13?

Swali la 3: Soma Wafilipi 1:6. Mungu anapanga kukusadia ukue kwa muda gani?

Swali la 4: Soma 2 Wakorintho 8:11 (chini hapa). Ni mambo gani matatu mistari hii inatuambia kuhusu malengo?

2 Wakorintho 8:11 (Swahili Union Version)

Lakini sasa timizeni kule kutenda nako, ili kama vile mlivyokuwa tayari kutaka, vivyo hivyo mkawe tayari na kutimiza, kwa kadiri ya mlivyo navyo.

A.____________________________________________________________

B.____________________________________________________________

C.____________________________________________________________

| | |
|---|---|
| Swali la 5: | Soma 1 Nyakati 28:20 (hapa chini). Ni sehemu gani ya mstari huu ni ya msaada kwako? Fafanua.<br><br>1 Nyakati 28:20 (Toleo la Swahili Union)<br><br>Kisha Daudi akamwambia Sulemani mwanawe, Uwe hodari, mwenye moyo mkuu, ukatende hivyo; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa BWANA, Mungu, Mungu wangu, yu pamoja nawe; yeye hatakupungukia wala kukuacha, hata itakapomalizika kazi yote ya huo utumishi wa nyumba ya BWANA. |

**11. Jadili hoja ndogo a: "Tafuta kile Mungu anataka ufanye"
(Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 15)**

Ili kuwapa wanafunzi mwelekeo wa tunakotaka kwenda katika kikao hiki, wape maswala yaliyoorodheshwa katika hoja ndogo a: *"Tafuta kile Mungu anataka ufanye"* katika ukurasa wa 15 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi. Kufuatana na mapendezi na haja za wanafunzi wako, unaweza kuchukua dakika chache kuelezea kwa kina ni nini "Mapenzi ya Mungu"

Baadhi ya wanafunzi wako huenda wasijue mafundisho msingi ya Kibiblia kwamba Mungu ana mipango kwa kila mwana wake. Kama bado haujafanya hivyo, chukua muda kujadili ukweli halisi wa Waefeso 2:10 na Yeremia 29:11

**Waefeso 2:10 Toleo la Swahili Union
Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.**

**Yeremia 29:11 Toleo la Swahili Union
"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho."**

Hatuna uhuru tu kupitia maisha tukifanya lolote tutakalo.

Inatupasa kujua kwamba kwa vile Mungu ndiye Kiongozi wa maisha yetu, ni sharti tumsikilize na tutambue anachotaka tufanye. Swala ya kutafuta mapenzi ya Mungu pia limejadiliwa katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya, Utiifu kwa Mungu.*

**12. Jadili hoja ndogo b, "Aina tofauti za malengo"
(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 16)**

Waulize wanafunzi waorodheshe aina tofauti ya malengo anayoweza kuweka Mkristo. Tazama hoja ndogo b, *"Aina tofauti za malengo,"* katika ukurasa wa 16 kwenye Mwonozo wa Wanafunzi kwa mawazo machache. Epuka majadiliano marefu kwa sasa. Lakini toa vielezi kadhaa vya malengo haya kutoka kwa maisha yako au ya wengine kuhakikisha kuwa wanaelewa tunachokizungumzia katika sehemu hii.

**13. Jadili hoja ndogo c, "Unawezaje kuanza kuweka malengo?"**
**(Dakika 15-25 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 16-18)**

Baadhi ya wanafunzi wako huenda hawajazoea kuweka malengo kwa usaidizi wa Mungu. Rejelea maandiko makuu kufikia hapa. "Tunapaswa kufanya mpango – tukimtegemea Mungu kutuelekeza" (Mithali 16:9 Toleo la Swahili Union). Ni nadra sana kwa wakristo kumsikia Mungu akizungumza kwa sauti kuu na kuwapa orodha ya malengo maishani. Hata hivyo, tunapoomba na kutazamia Biblia kwa msaada, tunaweza kuanza kufanya maamuzi yanayomridhisha Mungu.

Huenda ikawa ngumu kwa wanafunzi wako kuweka malengo fulani ya maisha kwa wakati huu. Lakini, sote tunaweza kuanza kuweka malengo ya muda mfupi au ya kila siku. Mwongozo wa mwanafunzi unatupatia mpangilio wa hatua sita za kuweka malengo ya kila siku. Tazama ukurasa wa 17-19 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

A. Kwa upesi taja kila mojawapo ya hatua sita zilizoorodheshwa katika ukurasa wa 16-18 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

B. Kisha rudi na kisha utoe vielezi 2 au 3 vya jinsi wewe mwenyewe au Mkristo mwingine mpya alifuata mfumo huu.

C. Mojawapo ya maswala tunayotaka washike ni jinsi ya kuhusisha malengo yao ya kila siku kwa Biblia. Malengo yao yanapaswa kusaidia kuunganisha sehemu hizi mbili.

**Unawezaje kuanza kuweka malengo?**

1. Angalia shida katika maisha yako ya kila siku.
2. Jiulize, "Je! Mungu anajaribu kunifundisha kufanya nini leo katika eneo hili la maisha yangu?
3. Tafuta eneo moja la maisha yako ambapo unataka kukua leo.
4. Unganisha utafiti wako wa Biblia kwa eneo hili ambalo unataka kukua.
5. Orodhesha vitu unavyoweza kukamilisha leo.
6. Tathmini matokeo.

*Nukuu toka kwa Mwongozo wa mwanafunzi ukurasa wa 16-18*

**14. Jadili hoja ndogo 6, "Tathmini matokeo"**
**(Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 17-18)**

Hatua ya mwisho katika kuweka malengo ni *"Tathmini matokeo."* Toa mifano kadha jinsi unnavyotathmini matokeo ya majaribio yako katika kutimiza malengo yako. Iwapo umeona nyenzo za *Mafunzo ya Kibinafsi kwa Maisha Mapya*, unaweza kutazama mazoezi kutoka 201-206, ambayo yako na maswali ya kutumia unapotathmini malengo timilifu.

Sisitiza haja ya usawaziko katika kuweka malemgo na vile vile kuyatimiza. Tunapaswa kuwa waangalifu kutilia mkazo vipaumbele. Malengo ni vifaa vinavyotusaidia kuwa watu anaowataka Mungu.

Inatupasa pia kuchukua muda kutathmini malengo yetu ya muda mrefu. Wahimize wanafunzi kuweka malengo ya muda mrefu na kuyarejelea mara kwa mara – angalau mara moja kwa miezi kadhaa. Tambua tathmini ya Yesu ya malengo yake ya maisha kabla ya kusulubiwa. Tazama Yohana Sura 17.



**15. Jadili hoja ndogo d, Alama nzuri ya kila siku ni ipi?**
**(Dakika 10-20 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 18-19)**

Kwa haraka, taja alama 6 za lengo zuri la kila siku. Kisha chukua malengo mawili au matatu nalo darasa litathmini moja baada ya lingine ili kuona kama yanaafikiana na vigezo vya lengo zuri la kila siku.

**Alama ya lengo zuri la kila siku**

1. Ni rahisi
2. Ni maalum
3. Ni la maana
4. Inatekelezeka
5. Inaweza kupimwa
6. Ina manufaa kwangu

*Nukuu toka kwa Mwongozo wa mwanafunzi, ukurasa wa 18-19*

Iwapo wanafunzi wako wanatumia pia *Mafunzo ya Kibinafsi kwa Maisha Mapya,* watakuwa na malengo mbalimbali binafsi ya kutathmini. Watazame malengo yao binafsi waliyoweka katika *Darasa la ukariri wa maandiko* na *Darasa la ubora wa hulka.*

Chukua malengo mawili au matatu na kuyarejelea darasani ili kuonyesha vizuri alama za malengo mazuri ya kila siku.

**16. Matumizi binafsi (Dakika 5-10)**

**A. Kuweka malengo ya kila siku**

Angazia matumizi binafsi jinsi wanavyoweza kuanza kuweka malengo ya kila siku. Rejelea ukweli halisi wa kibiblia na andiko kuu la leo. Pia waangalie waliyoyaandika katika swali la 7 katika Mwongozo wa somo, Zoezi la 2, **“Orodhesha baadhi ya maeneo katika maisha yako ambako unataka kukua.”**

**B. Zoezi la 3, “Kuweka Malengo katika Matendo”**

Eleza Mwongozo wa somo, Zoezi la 3, *“Kuweka Malengo katika Matendo,”* kufikia hapo, na uwaonyeshe jinsi inavyohusiana na kazi yao katika swali la 7 kutoka kwa Zoezi la 2. Hawapaswi kutumia mojawapo ya majibu yao kutoka Zoezi la 2 wanapomaliza Zoezi la 3, lakini wanaweza kufanya hivyo kwa hiari yao.

**C. Kuweka malengo ya muda mrefu**

Tendo lingine la matumizi binafsi ni kuwafanya wanafunzi watengeneze orodha ya malengo ya muda mrefu katika maisha yao. Wahimize kusali hima kuhusu malengo haya.

**17. Kazi za ziada**

A. Sahihisha Mwongozo wa somo Zoezi la 2, *"Malengo katika Biblia."*

B. Wanafunzi wako wamalize Mwongozo wa somo Zoezi la 3, *"Kuweka Malengo katika Matendo,"* baada ya kikao cha leo cha darasa.

C. Wanafunzi wasome Sura ya 2 katika mwongozo wao na warejelee waliyoyapitia katika darasa la leo kisha wajiandae kwa somo lifuatalo.

**18. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 3
# Dhibiti hisia zako

3

**1. Kweli Kuu ya Kibiblia:**

Ninahitajika kutambua jinsi Mungu anavyonitaka mimi kuonyesha hisia zangu.

**2. Mstari Mkuu: 1 Wakorintho 10:29 (Toleo la Swahili Union)**

Jinsi anavyohisi mtu mwingine ni muhimu. Hatuna uhuru wa kufanya mambo yatakayowadhuru watu wengine.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Ukurasa wa 19-25 katika Mwongozo wa Mwanafunzi na Mwongozo wa somo Zoezi la 4, *"Hisia zangu,"* zinaambatana na somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5-10)**

Anzisha kikao hiki cha darasa kwa kutoa kielezi cha ujenzi na makaazi katika nyumba. Unaweza kutumia hiki kielezi kuonyesha uhusiana kati ya imani, mambo ya hakika, na hisia katika maisha ya kila siku ya Kikristo.

**Jinsi ya kutumia kielezi hiki**


Lengo kuu la somo hili ni kuonyesha jinsi hisia zako huathiri maisha yako ya kila siku ukiwa Mkristo. Kujenga nyumba na kuishi ndani yake huweza kulinganishwa na kinachostahili kuishi maisha ya fanaka kama Mkristo.

**Ujenzi wa Nyumba**

Je, hisia zako ziko na umuhimu gani unapokuwa Mkristo? Je, Mungu anataka uyapuuze ? La ! Lakini zinapaswa kuchukua nafasi ya tatu. Kwanza kabisa, kuna mambo hakiki katika Biblia ambayo hukueleza jinsi ya kuwa Mkristo. Pili ni ile imani (nguvu) Mungu hukupa kutenda kulingana na yale mambo hakiki – kuyatii na kuwa Mkristo.

Hebu tulinganishe vitu hivi vitatu – mambo hakiki, imani, na hisia – na nyumba. Msingi wa nyumba unaashiria mambo hakiki katika Biblia, ambayo hutuambia jinis ya kuwa Mkristo. Nyuta, paa, dirisha n.k.., vinaashiria ile Imani anayotupatia Mungu kuwa Wakristo. Anatupatia nguvu za kubadilisha maisha yetu. Tunaweza kuona tofauti. Hisia zetu zinaweza kulinganishwa na joto ndani ya nyumba. Hisia zetu hutuwezesha kufurahia kila siku, jinsi vile joto hukufanya uhisi vyema katika msimu wa kipupwe.

Hisia zetu ni muhimu sana kwa sababu Mungu alituumba tuwe wasikivu na watu wenye hisia. Lakini jinsi unavyohisi unapokuwa Mkristo si muhimu kama kuelewa na kutii mambo hakiki katika Biblia ambayo hukuambia jinsi ya kuwa Mkristo.




**Kufanya nyumba yako kuwa tulivu**

Katika pembe nyingi za dunia, hali ya hewa hugeuka mwezi baada ya mwezi. Tuseme kwa mfano nyumbani mwako mna tanuu na kiyoyozi. Sababu kuu ya kuwa na vifaa hivi viwili ni kudhibiti vipimo vya joto viwe kwenye viwango vifaavyo mwaka mzima. Tunatumia moto kukiwa kuna baridi nje na kiyoyozi panapo joto jingi mno nje.

Cha msingi katika kuwa na nyumba tulivu ni kuwa mwangalifu kwa tanuu au kiyoyozi. Usipokuwa mwangalifu, na kuacha tanuu iwe moto kupindukia, moto unaweza kuzuka na kuchoma nyumba.

Ili kuzuia hili kufanyika, unaweza kuizima tanuu na kutoitumia kabisa. Nyumba labda haitachomeka lakini mabomba yanaweza yakaganda au wewe ukagwaya kwa baridi ikikithiri.

**Matumizi**

Mungu alikupa hisia ili uzifurahie. Anakupa jukumu la kujifunza jinsi ya kuzidhibiti vyema.

Kuhisi kuwa karibu na Mungu hakukufanyi kuwa Mkristo. Nyumba ni nyumba kuwepo na joto au la. Ni sawia na kuwa mkristo. Watu huwa Wakristo kwa sababu wamejenga misingi dhabiti ya maisha yao na “vitu” anavyowapa Mungu. Hisia nzuri hazikufanyi kuwa Mkristo. Lakini kuwa mkristo mwenye mafanikio, ni lazima kujifunza kudhibiti hisia zako vyema.

Usipokuwa mwangalifu na hisia, waweza kukumbana na madhara makubwa mno, sawia na kutokuwa mwangalifu na tanuu nyumbani mwako. Moto huenda ukachoma nyumba. Ukiaziachilia hisia zako zikawa legevu, unaweza kuishia kuharibu uhusiano wako na Mungu. Kwa mfano, Ken alimkasirikia mtu na kuzua vita. Baada ya vita, Ken bado alikuwa na makasiriko. Tamaa yake ya kisasi ilimtenganisha na Mungu.

Baadaye aliwazia tukio hilo zima na kuamua ya kwamba, kama Mungu asingalimtolea hasira, basi Ukristo usingalimfaa.

Kumlaumu Mungu hakutamtatulia Ken tatizo lake. Mkristo mwenye mafanikio hujifunza kudhibiti hisia zake vyema.

Wakristo wengine hutenda kinyume na alivyotenda Ken. Wanafahamu kwamba ni makosa kuruhusu hisia kudhibiti maisha yao. Kwa hivyo hukandamiza hisia zao. Wakristo hawatayafurahia maisha ikiwa watakataa hisia zozote changamfu kujaza mioyo yao. Watakuwa watu baridi na wasio na hisia-moyo.

3

Watu wengine huwa na wazo kuwa wakristo halisi wa kiroho huwa hawaonyeshi hisia zao waziwazi. Uchunguzi wa makini katika maisha ya Yesu unadhihirisha kwamba msimamo huo si kweli. Katika matukio mengi, Yesu alionyesha wazi hisia Zake.

Wakristo wengine hujaribu kudumisha uhusiano wao na Mungu kupitia hisia zao. Wanapohisi kuwa karibu na Mungu leo, wanashawishika kwamba wanaimarika kiroho. Msingi wa aina hii huja kuwa dhaifu mno. Hisia zetu hubadilika siku baada ya siku. Hisia zijengapo msingi wa uhusiano wako na Mungu, basi nguvu (au uthabiti) wa uhusiano wenu pia utabadilika siku baada ya siku. Ni lazima uyajenge maisha yako juu ya msingi wa ukweli wa kibiblia – wala si hisia zako.

### 5. Kusudi la somo hili

Elezea kusudi kuu la somo hili la hisia. Fafanua tofauti kati ya somo hili na lile la hisia katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya*, *Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?* Katika kozi hiyo, lengo kuu ni kufafanua jinsi hisia huhusika tunapokuwa wakristo. Katika somo hili, lengo kuu ni kuangazia jinsi hisia hufanya kazi katika maisha ya kawaida ya Mkristo mwenye mafanikio.

Nyenzo kabambe inayohusiana na hisia ni kitabu, Uponyaji kwa Hisia Zilizoharibika (*Healing for Damaged Emotions),* kilichoandikwa na David Seamands. Toleo hili la daftari liko na kitabu kizima pamoja na sehemu yenye maswali ya kusoma na kutafakari. Unaweza kusoma kitabu hiki na kuwahimiza wanafunzi kukisoma iwapo wamepitia hali ya uchungu katika maisha yao ya zamani.

### 6. Ukweli wa kimsingi kuhusu hisia zetu (Dakika 3-5)

Kufikia hapa, unaweza kutoa taarifa ya jumla kuhusu hisia.

A. Hisia ni muhimu kwa wakristo.

B. Mungu alituumba tukiwa na hisia. Anataka tujifunze jinsi ya kuonyesha hisia zetu kwa njia ambazo zitamridhisha.

C. Hisa zetu hubadilika, wakati mwingine haraka sana. Hii ni kawaida.
Na ni SAWA – angalau wakati mwingine!

D. Hisia zetu hazifai kuwa msingi wa uhusiano wetu na Mungu. Siku nyingine unaweza kuhisi uwepo wa Mungu karibu nawe. Wakati mwingine unaweza kuhisi kana kwamba Mungu amekuacha pweke.

E. Wakristo wenye mafanikio hujifunza kuwa wasikivu na kutanabahi hisia zao na za wengine vile vile.

**7. Jinsi Yesu alivyoonyesha hisia Zake (Dakika 10-20)**

Katika tendo lifuatalo, gawanya darasa kwa vikundi vidogo (wanafunzi wawili hadi wanne kwa kila kikundi). Tanguliza tendo hili kwa kueleza kwamba katika matukio kadha, Yesu alionyesha wazi hisia Zake.

**A. Tendo la kikundi kidogo (Dakika 5-10)**

Kipe kila kikundi mojawapo ya vifungu vifuatavyo vya Biblia. Wasome na kutambua hisia alizozionyesha Yesu katika kila tukio. Mbona Yesu alionyesha hisia hii?

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Marko 10:17-30 | Mtu aliyekuwa tajiri | Mstari 21. Upendo |
| 2 | Yohana 11:1-44 | Kifo cha Lazaro | Mstari 33-35 Huzuni |
| 3 | Marko 3:1-6 | Yesu amponya mtu mwenye mkono uliopooza | Mstari 5. Hasira |
| 4 | Marko 6:30-44 | Yesu awalisha watu 5000 | Mstari 34. Rehema |
| 5 | Marko 15:16-39 | Kusulibiwa kwa Yesu | Mstari 34. Maumivu |

**B. Ripoti za vikundi vidogo**

Kila kikundi kiripoti matokeo kwa darasa zima. Kwanza waeleze kwa ufupi hadithi – hali aliyojipata Yesu. Waeleze pia ni hisia zipi Yesu alizozionyesha na jinsi alivyozionyesha (kama maandiko yanasimulia). Wanapoelezea **kwa nini** Yesu alionyesha hisia hii, wanapaswa kuliambia darasa kama Biblia inakariri hili, ama kama ni maoni ya kikundi kutokana na habari inayotolewa na maandiko.

**C. Mukhtasari na lengo la tendo hili.**

Tumia tendo hili huelezea kwamba Yesu alionyesha hisia Zake kwa njia za kistaarabu na zinazotangamana na Biblia. Kama Wakristo wapya, tunapaswa kulenga shabaha la kuonyesha hisia zetu kwa njia zitakazomridhisha Mungu.

**8. Tambulisha Hatua ya 4, "Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako"**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 19-21)**

Tanguliza hatua 4 kwa kuorodhesha na kurejelea haatua 3 za kwanza za kuwa mkristo mwenye mafanikio. Unaweza kutumia maarifa yalitwaaliwa katika ukurasa wa 19-21 wa Mwongozo wa Mwanafunzi, kutanguliza hatua ya 4 *"Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako"*. Neno muhimu hapa ni "dhibiti". Kudhibiti ni kutumia kwa njia bora na kwa wakati mwafaka.

Uthabiti mzuri wa hisia zako haumaanishi kuzikandamiza au kuzipuuza. Kujifunza jinsi ya kudhibiti hisia kunahusisha kujua jinsi ya kuzitumia hisia zako vyema.

Unaweza kuchukua muda mfupi kujadili swali la 1-3 kwa Zoezi la 4, "Hisia Zangu." Maswali haya yanawauliza wanafunzi kuangalia kinachosemwa na Biblia kuhusu baadhi ya hisia tulizo nazo.

Swali la 3 pia linaweza kutumika unapojadili kuhusu utakachofanya “hisia zisizo sawa” zinapoibuka. Eleza kwamba jinsi vile Yesu alivyoonyesha hisia Zake, Mungu anatutaka nasi pia tushuhudie manufaa kamili ya kutumia hisia zetu kwa njia zinazofurahisha.

***Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi 4 “Hisia zangu”***

1. Soma 2 Wakorintho 8:11 kutoka kwa Toleo la Swahili Union.
   Ni hisia ya aina gani unapaswa kuonyesha unapofanya kazi yako?

   2 **Wakorintho 8:11 Toleo la Swahili Union**

   Lakini sasa timizeni kule kutenda nako, ili kama vile mlivyokuwa tayari kutaka, vivyo hivyo mkawe tayari na kutimiza, kwa kadiri ya mlivyo navyo.

2. Ni aina gani ya hisia Mungu anatarajia kutoka kwa maisha yako?
   A. Marko 12:30-31________________________________________
   B. Yohana 14:27________________________________________
   C. 1 Petro 1:16; 1 John 1:4________________________________
3. Ni aina gani ya hisia ambayo haipaswi kutawala maisha ya Mkristo?
   A. 2 Timotheo 1:7________________________________________
   B. Yakobo 1:19-20________________________________________
   C. Hatia

3

Basi ni vipi Mkristo mpya anaweza kujifunza kudhibiti hisia zake jinsi Yesu alivyofanya? Mambo matatu yametolewa katika Mwongozo wa Mwanafunzi katika ukurasa wa 20-21 (hoja ndogo a-c)

**9. Jadili hoja ndogo a, “Unajifunza kudhibiti hisia zako kwa kukuza mitazamo yenye msingi wa Maandiko.”**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 20)**

Katika kupitia swala hili, hakikisha kwamba wanafunzi wako wanafahamu tofauti kati ya mitazamo na hisia. Sisitiza umuhimu wa mafunzo ya Biblia kufikia hapa.

Sisitiza ukweli kwamba hisia zetu tumezipata toka kwa Mungu na angetaka tuzishuhudie kwa haki. Wakati mwingine wakristo huwa na wazo kuwa wale wanaoonyesha hisia zao wazi wanadhihirisha jinsi hawajakomaa. Yeu anatoa mfano wazi kwetu. Anaonyesha hisia Zake wazi.

Mtu anapokuwa Mkristo, yeye hastahili kujaribu kuwa mtu tofauti kabisa. Mungu hataki uache kuwa na haiba yako. Anataka uasi njia zako za dhambi zinazozuia kuimarika kwako kiroho.

Wakristo wasioonyesha hisia zao hawadhihirishi “ukomavu wa kweli wa kiroho”. Kama wewe ni mtu mwenye “hisia baridi,” na mwenye kuonyesha hisia kwa nadra, basi Mungu anataka uwe kama Kristo. Huku kuna maana ya kujifunza njia bunifu za kuonyesha hisia zako ili wenzako waje kujua kwamba u “mtu mchangamfu.”

Wakristo wengine ni wepesi wa kujionyesha na huruhusu hisia zao kutawala maisha yao. Iwapo watataka kumrithi Kristo, basi itwabidi kujua jinsi ya kudhibiti hisia zao.

Hisia, chimbuko lake ni akili. Jinsi tunavyotenda na hisia zetu hutegemea mitazamo yetu. Iwapo twataka kuhisi anavyohisi Mungu, lazima kwanza tujifunze kufikiria kama Mungu. Jifunze njia njema za kuonyesha hisia zako. Jifunze kutendea kila hali na hisia ambazo angezitumia Yesu katika hali kama hiyo.

Kama ulikuwa umefunza kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* yenye mada *Mitazamo*, unaweza kuonyesha kwa ufupi jinsi maswala yote yaliyosomwa katika somo hilo yanahusiana na hatua hii ya kuwa Mkristo mwenye mafanikio.



**10. Jadili hoja ndogo b, Unapokuwa na "hisia zisizo sawa" zipeane kwa Mungu kupitia sala. (Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 20-21)**

Fanya muhktasari wa hoja kuu zilizoangaziwa katika Mwongozo wa mwanafunzi, haswa kinachofanya hisia iwe "mbovu?'' Unaweza kutumia swali la 3 katika mwongozo wa somo zoezi kufikia hapa: **"Ni aina gani ya hisia ambayo haipaswi kutawala maisha ya Mkristo?"** Taja kwamba katika baadhi ya Zaburi, Mfalme Daudi anaonyesha hisia kwa Mungu. Mara nyingi yeye alimwambia Mungu kuhusu hamaki na chuki alizokuwa nazo kwa maadui wake.

Hisia zisizofaa, zilizo nadra, kama inawezekana, husaidia hali kuwa bora. Kwa hivyo unaweza pia kujifunza kutenda jinsi Yakubu 1:2 inakariri – Jibu kwa furaha. Ukikuza mtazamo huu katika hali yoyote ile, itakuwa rahisi kwako kurejea kwa furaha katika kila hali.

**11. Hisia zetu na majaribu ya kutenda dhambi (Dakika 5-10)**

Unaweza kuchukua muda fulani na kujadili baadhi ya hali ambapo wanafunzi wako hupata majaribu kuonyesha hisia zisizofaa na kwa wakati usiofaa. Mfano mzuri ni wakati mtu anakukosoa au kukukashifu. Mara aghalabu itikio lako la hisia-moyo huwa na hasira au hofu. Yoyote kati ya hisia-moyo hizi huweza kwa urahisi kuwa na msukumo wa hata kutamka au kufanya mambo utakayojuta baadaye.

Kinyume kinaweza kuwa kweli tunapokabiliwa na kishawishi kutenda dhambi. Mvuto wa kihisia kwa kishawishi hicho huenda ukawa hisia zuri. Kwa mfano, kumbukumbu za jinsi ilivyohisi kuwa mlevi na madawa ya kulevya huweza kuwa msukumo mkuu wa kumrudisha mtu tena katika tabia ya ulevi.

Au pia, uhusiano wa kihisia wa urafiki wa jadi unaweza kusalia moyoni kwa muda mrefu, hata ingawaje mtu huyo si Mkristo. Hizi "hisia nzuri" kwa mtu huyu zinaweza kuwa zinakuvuta katika uhusiano unaoenda kinyume na matakwa ya Mungu kwako.

Katika kitabu cha Kutoka Sura ya 3, Hawa alihisi mvuto wa kihisia kwa lile tunda ingawa alikuwa ameamriwa na Mungu asilile. Hii ni mifano ambapo "hisia zetu" zinaweza kuwa zinatupotosha – mbali na Mungu, badala ya kuwa karibu naye.

Tunapaswa kujifunza kutumia ukweli wa Mungu kama kengele ya kututahadharisha hisia hizi zinapojaribu kuturai kuwa kwa hali ya dhambi.

**12. Jifunze jinsi ya kuelezea hisia zako kwa maneno (Dakika 5-10)**

Katika kipindi hiki chote, sisitiza umuhimu wa kujifunza kueleza hisia zako. Watu wengi hawajawai kujifunza kufanya hivi – haswa kwa njia komavu. Katika kitabu chake, Ni kwa Nini Nina Hofu ya Kukwambia Mimi ni Nani? (*Why Am I Afraid to Tell You Who I Am?,* John Powell yuko na sura (#4) mufti sana kuhusu Kushughulikia Hisia (Zetu*"Dealing with Our Emotions.")* Anatoa mifano mizuri sana ya njia mwafaka na zisizofaa za kuelezea hisia.

**13. Jadili hoja ndogo c: Jifunze kujwa msikivu kwa hisia za watu wengine (Dakika 10-15, Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 21)**

3

Toa mukhtasari wa hoja kuu kuhusu mada hii ilivyoangaziwa katika Mwongozo wa mwanafunzi. Swali la 4 katika mwongozo wa somo zoezi la 4 pia linaambatana na mada hii.

***Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 4, "Hisia zangu.***

4. 2 Wakorintho 10:29 katika Biblia ya Toleo la Swahili Union inasema, "Nasema, dhamiri, lakini si yako, bali ya yule mwingine. Maana kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu mwingine?"

   Njia nyingine ya kuelezea kile mstari huu unasema ni kwamba: "Jinsi yule mtu mwingine anavyohisi ni muhimu. Hatuko huru kufanya mambo yatakayowaletea wengine machungu."

   A. Unaweza kufikiria kuhusu hali katika siku chache zilizopita ambapo ulifanya kitu ambacho kilimfanya mtu kuwa na uchungu? Elezea kwa kifupi.

   B. Ulikuwa unajihisi vipi katika hali hiyo?

   C. Je, unafikiria yule mtu alijihisi vipi wakati au baada ya hali hiyo?

   D. Je, ungeitikia vipi kwa tofauti ili yule mtu asihisi uchungu?

Kama wanafunzi wanachelea kutumia majibu yao binafsi katika swali hili, unaweza kuwapa mifano kadhaa kutoka kwa maisha yako na mingine ya wanafunzi wa hapo awali.

La kusikitisha ni kuwa, hakuna hatua za kimuujiza zitakazokupa usikivu huu kwa mpigo. Wengine wetu wamekuwa wasiojali kabisa hisia za wengine. Msururu wa mahusiano yaliyoharibika nyuma yetu unaonyesha matokeo ya mtindo huo wa kuishi. Andiko kuu la leo linaangazia hoja hii. Chukua muda kujadili jinsi unavyoweza kuwa msikivu kwa hisia za wengine.

**14. Uponyaji hisia zilizoharibiwa (Kwa hiari – dakika 10-20)**

Ukiwa na muda, unaweza kujadili swala la uponyaji wa hisia zilizohariwa. Wakristo wengi wanatoka katika mazingira ambapo walikumbana na madhara ya hisia-moyo, mara nyingi katika muktadha wa mahusiano ya kijamii. Baadhi ya madhara haya huenda yakawa na kina kirefu na hivyo yakawa na athari kubwa kwa uwezo wa kutenda matendo kama Mkristo. Uponyaji wa ndani wakati mwingine huwa jambo la mtafaruku katika madhehebu, kwa hivyo ni lazima utathmini njia mwafaka ya kujadili swala hili darasani.

David Seamands ameandika kitabu kuhusu swala hili. *Healing for Damaged Emotions* (Victor Books). Kitabu cha mazoezi kipo pamoja na maswali ya somo na tafakari binafsi.



**15. Vidokezo vya mazoezi zaidi kwa vikao vya darasani.**

Iwapo ungependa kuchukua muda zaidi katika swala hili, unaweza kujadili kwa mapana na marefu hisia mahsusi zilizo ngumu kwa wakristo. Kitabu cha James Dobson, *Emotions: Can You Trust Them?* kinatoa maelezeo sharifu kuhusu swala hili. Kuna vitabu vingi vingine vizuri kuhusu hisia.

**16. Jadili hatua ya 5, Wafahamishe wengine kile Kristo amefanya katika maisha yako.” (Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 22)**

Kuelekea mwisho wa darasa hili, jadili kwa kifupi hatua 5, “*Wafahamishe wengine kile Kristo amefanya katika maisha yako.*” Hii ni hatua ya muhimu sana kwa Wakristo wapya. Kujifunza kuwafahamisha wengine alichokifanya Mungu katika maisha yako ni njia madhubuti ya kuimarika katika uhusiano na Yesu. Ukiwa na muda, unaweza kufanya kando kikao cha darasa kuangazia hatua 5. Tazama ukurasa 22 katika Mwongozo wa mwanafunzi kwa maelezo zaidi kuhusu mada hii.

**17. Jadili Hoja B: “Jinsi ya kuanza kutumia hatua hizi tano”**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 23-25)**

Unapohitimisha somo hili, jadili kwa ufupi vidokezo vya jinsi ya kuanza kutumia hatua hizi 5 kuwa mkristo mwenye mafanikio. Sisitiza umuhimu wa matumizi binafsi – sio tu mara moja au mara mbili – bali mfululizo, siku baada ya siku.

Kadri wanavyojitahidi kuziweka hatua hizi kwa matendo, ndivyo watakakvyoingia katika uhusiano wa dhati na Yesu.

**18. Matumizi binafsi (Dakika 5-10)**

**A. Onyesha hisia zako kwa haki**

Angazia matumizi binafsi leo kwa kuziweka hisia zako kwa manenoo – kwa Mungu na wengine. Sisitiza umuhimu wa kuwa mnyoofu kwa hisia zako. Walioimarika kiroho huwa hawakani hisia zao. Wako adili kuhusu hisia hizi na huzionyesha kwa njia zinazomfurahisha Mungu. Unaweza kuwakubalia kutazama jibu waliloandika kwa swali 5 kwenye Mwongozo wa somo zoezi 4.

**B. Kujifunza kuwa wasikivu kwa wengine**

Sehemu nyingine muhimu ambayo inaweza kuwa angazio la matumizi binafsi ni kuwapa changamoto wajifunze kuwa wasikivu kwa hisia za wengine.
Unaweza kuwaambia wamchague mtu mmoja ambaye wangetaka kumwonyesha usikivu. Waandike vitu viwili wanavyoweza kufanya kwa siku chache sijazo kuonyesha kujali maslahi ya mtu huyo.

**19. Kazi za ziada**

A. Mwishoni mwa darasa, toa swali kuhusu 1 Wakorintho 10:29

B. Sahinhisha Mwongozo wa somo Zoezi la 4, *"Hisia zangu"*.

C. Sahihisha Mwongozo wa somo Zoezi la 3, *"Kuweka Malengo katika Matendo"* aidha leo au baada ya kikao kifuatacho.

D. Waelekeze wanafunzi kusoma sura ya 3 katika Mwongozo wa mwanafunzi wakijitayarisha kwa kipindi kifuatacho.

**20. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo la 4
# Roho Mtakatifu



**1. Kweli Kuu ya Kibiblia**

Inanipasa kumruhusu Roho Mtakatifu kuwa mwalimu wangu ili niwe Mkristo mwenye furaha na mafanikio.

**2. Mstari Mkuu: Yohana 16:13 Biblia ya Toleo la Swahili Union**

Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 3 katika Mwongozo wa mwanafunzi na Mwongozo wa somo Zoezi la 5, “Roho Mtakatifu ni nani?” na Zoezi la 6, “Roho Mtakatifu maishani mwangu” zinaambatana na somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5-10)**

Anza somo la leo kwa kuwaagiza wanafunzi washirikishe majibu yao ya maswali 1 na 2 katika mwongozo wa somo zoezi la 6.

**Kutoka Mwongozo wa somo Zoezi la 6. “Roho Mtakatifu maishani mwangu”**

Swali 1: Fikiria nyuma kile ulichofahamu kumhusu Mungu miezi sita iliyopita. Wakati huo, mawazo au imani yako kuhusu Roho Mtakatifu ilikuwa nini?

Swali 2: Elezea jinsi mawazo na imani yako kuhusu Roho Mtakatifu imebadilika ndani ya miezi sita iliyopita.

Majibu yao kwa haya maswali yanaweza kukupa ufahamu mwema kuhusu maswali yanayohitaji kuangaziwa katika kikao cha somo la leo.

**5. Jadili Hoja A: Roho Mtakatifu ni nani?**
**(Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 26-27)**

Tumia zile nyenzo katika Mwongozo wa mwanafunzi, ukurasa wa 26-27 kuunganisha majibu tofauti walioyatoa wanafunzi katika tendo la mwanzo (#4 juu hapa). Huenda ukahitajika kuelezea dhana ya Utatu Mtakatifu ndipo wanafunzi wapate kuona kwamba Roho Mtakatifu yu katika uhusiano na Yesu pia na Mungu Baba. Hakikisha kwamba hawamrejelei Roho Mtakatifu kama chombo.
Yeye ni kiumbe hai.

Swali la 1 kutoka kwa Mwongozo wa Somo, Zoezi la 5 linaweza likatumika pia kufikia hatua hii.

> **Kutoka Mwomgozo wa somo Zoezi 5, "Roho Mtakatifu ni nani?"**
>
> Swali 1: Soma Yohana 14:15-17 katika Biblia yako.
> Ni majina yapi yametumiwa kumueleza Roho Mtakatifu katika mistari hii?

**6. Anachofanya Roho Mtakatifu leo katika dunia yetu. (Dakika 5-15)**

4

Tumia swali la 2 kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi 5 kuanzisha majadiliano kuhusu anachofanya Roho Mtakatifu duniani leo. Waulize wanafunzi watambue maswali yaliyoorodheshwa katika Yohana 16:6-11 kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu. Baada ya wao kufanya hivyo, taja kwamba Roho Mtakatifu yupo kazini katika maisha ya kila moja, wala sio wale walio Wakristo.

> **Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 5, "Roho Mtakatifu ni nani?"**
>
> Swali 2: Yesu alifafanua kile ambacho Roho Mtakatifu angefanya ulimwenguni baada ya Yesu kurudi mbinguni. Hata kabla mtu hajakuwa Mkristo, Roho Mtakatifu huwa anafanya kazi maishani mwake. Ni mambo gani matatu ambayo Roho Mtakatifu atatuonyesha? Soma Yohana 16:6-11. Andika mstari ambapo ulitoa jibu lako.

**7. Jadili Hoja B: Je! Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako unapokuwa Mkristo? (Dakika 10-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 27-29)**

Kabla ya kuanza kujadili masuala yaliyoibuliwa katika Mwongozo wa mwanafunzi, waruhusu wanafunzi kuwaambia wenzao majibu ya swali la 3 katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 5.

> **Kutoka Mwongozo wa somo Zoezi la 5, "Roho Mtakatifu ni nani?"**
>
> Swali 3: Soma Warumi 8:16. Roho Mtakatifu ana majukumu muhimu ya kufanya maishani mwako wakati unapofanya uamuzi wa kuwa Mkristo.
> Roho Mtakatifu anaahidi kufanya nini ndani yako wakati unapokuwa Mkristo?

Tumia nyenzo katika Mwongozo wa mwanafunzi, ukurasa wa 27-29, kufanya mukhtasari wa maswala yanayohusiana na kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo.

**B. Je! Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako unapokuwa Mkristo?**

1. Anakuhukumu dhidi ya dhambi
2. Anakuvuta kwa Kristo
3. Yeye huja na kuishi katika roho yako

*Nukuu kutoka katika mwongozo wa mwanafunzi, ukurasa wa 27-29*

Hakikisha wanaelewa kwamba Roho Mtakatifu huja na kukaa ndani ya mtu punde tu anapokuwa Mkristo. Wakristo wengine wako na dhana potovu kwamba Roho Mtakatifu huja na kukaa ndani yako baada ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Jaribu kuelezea kila hoja ndogo katika sehemu hii. Iwapo wanafunzi wanapata wakati mgumu kutafakari maelezo binafsi, toa mifano kutoka kwa maisha yako na yale ya wanafunzi wa awali.



**8. Panga ratiba yako kupitia Hoja C: Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako baada ya wewe kuwa Mkristo?**
**(Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 29-35)**

Kuna mengi unayoweza kuchagua unapofunza sehemu hii ya mwisho kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Wakristo. Kulingana na jinsi umepanga muda wako kwa sehemu nyingine ya somo hili ambalo tayari umeshalipitia, utakuwa na takriban dakika 15-30 kuyapitia maswala ibuka katika Hoja C ya somo hili.

Ikiwa kuna muda, unaweza kufanya zaidi ya vikao viwili vya darasa kuhusu Roho Mtakatifu. Ukitaka kupitia kwa kina Ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuna nyenzo maridhawa katika Mwongozo wa mwanafunzi zinazoweza kutumika katika kikao kizima cha mada hii. Unaweza pia kwa urahisi kutumia kikao kingine kupitia vipaji vya Roho Mtakatifu na kingine kwa matunda ya Roho Mtakatifu.

Miongozo mingine ya mpangilio wa somo kwa walimu umependekeza muda maalum wa kujadili kila mojawapo ya matendo haya. Kutegemea muda unaoruhusu katika sehemu hii ya somo, huenda ukahitajika kubadilisha kiwango cha muda kwa kila hoja katika mpangilio wako wa somo.

Ukurasa wa 29-35 katika Mwongozo wa mwanafunzi unatoa vigezo 6 vya kazi ya Roho Mtakatifu.

**C. Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha yako baada ya wewe kuwa Mkristo?**

1. Roho Mtakatifu hukusaidia kuwa Mkristo aliyefanikiwa.
2. Roho Mtakatifu atakusaidia kuelewa ukweli wa Mungu.
3. Roho Mtakatifu atakusaidia kupinga majaribu.
4. Roho Mtakatifu huzaa matunda yake maishani mwako.
5. Unaweza kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.
6. Hutoa karama za Roho Mtakatifu.

*Nukuu kutoka kwa Mwongozo wa mwanafunzi, ukurasa wa 29-35*

4

Maswali 4-9 katika Meongozo wa somo Zoezi la 5, “Roho Mtakatifu ni nani?” na masawli 3-6 katika Mwongozo wa somo Zoezi la 6, “Roho Mtakatifu maishani mwangu,” pia zinaambatana na sehemu hii ya somo. Utahitaji kupanga ni sehemu zipi utakazozipitia katika darasa kwa kutathmini kwa makini ukomavu wa kiroho wa wanafunizi wako na pia ufahamu wao wa Roho Mtrakatifu.

**9. Jadili Mwongozo wa somo Zoezi 5 (Dakika 5-10)**

Anza majadiliano ya mada hii kwa kuwauliza wanafunzi kusema majibu yao ya swali la 6 kuhusu Zoezi la 5, “Roho Mtakatifu ni Nani?” Kisha ujadili majibu yao kwa maswali ya 4,5, na 9.

**Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 5, “Roho Mtakatifu ni Nani?”**

Swali 6: Roho Mtakatifu hufanya nini katika maisha ya Wakristo?

A. Warumi 8:9 (mambo 2)____________________

B. Warumi 8:9____________________

C. Yohana 16:13____________________

D. Warumi 8:16____________________

> **Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 5, "Roho Mtakatifu ni Nani?"**
>
> Swali 4: Kulingana na Yohana 14:17, ni kwa njia gani tunafikia kumjua Roho Mtakatifu?
>
> Swali 5: Soma Yohana 14:25-27. Ni mambo gani mawili Yesu Kristo aliahidi Roho Mtakatifu atafanya kwa wale watakaomwamini?
>
> A. ____________________
>
> B. ____________________
>
> Swali 9: Soma Warumi 8:26-27. Ni kwa njia gani Roho Mtakatifu huwasaidia Wakristo?



**10. Jadili swali la 6A katika Zoezi la 6 (Dakika 5-10)**

Tumia swali la 6A katika Mwongozo wa somo Zoezi la 6, kujadili jinsi Roho Mtakatifu anatuongoza leo. Hakikisha kwamba zoezi hili ni kwa Wakristo wapya, na lisiangaziwe kwa mtazamo kwamba ni Wakristo wakomavu Kiroho pekee watakaoelewa.

> **Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 6, "Roho Mtakatifu Maishani mwangu."**
>
> Swali la 6A: Soma Yohana 16:13. Roho Mtakatifu atakufanyia nini?

Hii hapa mifano michache ya jinsi Roho Mtakatifu anatuongoza leo. Waagize wanafunzi wafahamishe wengine majibu yao kabla ya kuwapa yaliyoorodheshwa hapa chini. Toa maelezo mahsusi ya jinsi Roho Mtakatifu anavyotuongoza kupitia kila moja ya njia zifuatazo:

- Biblia
- Sala
- Ufahamu wako
- Mafikira yako
- Kupitia watu wengine

Unaweza kuwaruhusu wanafunzi washiriki na darasa, majibu yao ya swali 6B kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 6.

> **Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 6, "Roho Mtakatifu maishani mwangu."**
>
> Swali la 6B: Unaweza kufikiria kuhusu hali fulani katika maisha yako ambapo unajua Roho Mtakatifu alikuongoza katika kweli kuhusu jambo fulani? Fafanua kwa kifupi.

Wazo kuu zaidi katika sehemu hii ni kwamba Roho Mtakatifu anatuongoza kwa ukweli. Lakini sharti tuwe tunasonga iwapo atatuongoza. Roho Mtakatifu hatamuongoza mtu ambaye hataki kusonga. Lazima tutie jitihada kutekeleza ukweli wa Mungu katika maisha yetu ya kila siku. Tunapofanya matendo, Roho Mtakatifu anatuongoza katika ukweli wote.

**11. Jadili Hoja C-3: Roho Mtakatifu atakusaidia kupinga majaribu (Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 30)**

Swala la vishawishi ni nyeti sana kwa Wakristo wapya. Wanapaswa kukubali kwamba vishawishi vyenye uzito mkubwa vitawakumba hata wasiweze kuvistahimili kwa nguvu zao wenywe. Ni lazima Wakristo wapya wajifunze kumtegemea Roho Mtakatifu kwa nyakati kama hizi. Lakini lazima pia wajue anachowatarajia Mungu kufanya wanapokumbwa na majaribu. Tazama ukurasa wa 30 katika Mwongozo wa mwanafunzi kwa maelezo zaidi kuhusu mada hii muhimu.



**12. Jadili Hoja C-4: Roho Mtakatifu huzaa matunda yake maishani mwako (Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31)**

Anza majadiliano ya matunda ya Roho Mtakatifu kwa kuwauliza wanafunzi kuyatambua yaliyoorodheshwa katika Wagalatia 5:22-23. Warejelee majibu yao ya swali la 4 katika Mwongozo wa somo Zoezi la 6, ambalo liliwauliza waorodheshe matunda haya 9.

Kabla ya kuingia katika mjadala wa kina kuhusu matunda haya, chukua muda kuelezea maana ya Matunda ya Roho Mtakatifu.

**Mwongozo wa somo Zoezi la 6, “Roho Mtakatifu maishani mwangu”**

Swali 4: Wakati unapomruhusu Roho Mtakatifu kuongoza kukua kiroho, atakusaidia kuwa Mkristo anayezaa matunda. Ni maelezo yapi tisa yanayotumiwa kuelezea tunda la Roho Mtakatifu yaliyoorodhesha katika Wagalatia 5:22-23?

Baada ya kuorodhesha yote tisa, fikiria jinsi unavyodhihirisha yote haya katika maisha yako ya kila siku. Jipe alama ya 1 hadi 10 kwa kila tunda. Kuwa na alama 10 maishani mwako ina maanisha kufanikiwa, na alama 1 inamaanisha unahitaji kufanya bidii katika kutekeleza tunda hili la Roho Mtakatifu.

Katika kujadili matunda ya Roho Mtakatifu, zingatia ukomavu wa kiroho wa wanafunzi wako. Tumia muda wowote utakaohisi unatosha katika swala hili kwa sababu ya wanafunzi wako. Tazama ukurasa wa 31 katika Mwongozo wa mwanafunzi kwa maelezo zaidi.

**13. Jadili Hoja C-5: Unaweza kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu (Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzin ukurasa wa 31-34)**

Unaweza ukafikiria kuzingatia matukio binafsi ya wanafunzi wako unapopanga sehemu hii ya somo. Je, kunaye yeyote ambaye amepokea kipaji hiki? Unaweza kuanza sehemu hii ya somo kwa kuwaomba wakuambie maswali waliyo nayo kuhusu mada hii. Orodhesha maswali yao kwa ubao kisha uyatumie kama mwongozo wa kutathmini muda utakaoutumia kwa maswala tofauti yanayohusika na mada hii. Kama ratiba yako itakuruhusu, unaweza kumaliza kikao kizima cha darasa kwa mada hii.

Tumia maelezo katika ukurasa wa 31-35 kwenye Mwongozo wa mwanafunzi katika kuwasilisha mada hii. Unaweza kurejelea nyenzo kadhaa zilizoorodheshwa katika tovuti ya kozi hii. (tazama anwani ya tovuti ndani ya jalada la kitabu hiki). Kitabu kimoja chenye manufaa ni Kuzungumza Kwa ndimi: Hayo Nyiyo Yote Yalipo? (*Speaking in Tongues: Is That All There Is?)* cha Bob Cook (Gospel Publishing House).

**14. Maswali kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu (dakika 5-15)**

4

Hii hapa ni mifano ya maswali ambayo yameulizwa kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaweza kujumlisha orodha ya maswali ya wanafunzi wako kuhusu swala hili.

**(1) Je, ni lazima upokee ubatizo wa Roho Mtakatifu ili kuwa Mkristo mwenye mafanikio? Au ni lazima uweze “kunena kwa ndimi” ili uingie mbinguni?**

Jawabu kwa maswali yote mawili ni « la ». Lakini hebu tuyatazame maswali hayo, hususan la kwanza. Mbona sisi Wakristo huchagua mambo duni na bado tunafaulu kuingia mbinguni? Badala ya kuuliza ni vipi kati ya vipaji vyake Mungu tuavyoweza kupuuza au kuishi bila, tunapaswa kulishughulikia swala hili kwa mtazamo tofauti kabisa. Inatupasa kuwajibika kwa kuwa tayari kwa yote aliyo nayo Mungu kwetu. Ikiwa ubatizo wa Roho Mtakatifu unapatikana leo, basi ninapaswa kumjulisha Mungu juu ya ari yangu kwa vipaji hivi.

**(2) Je, ni lazima niweze “kunena kwa ndimi” ili nipokee ubatizo wa Roho?**

Mungu anataka kuwadibiti nyote. Yakubu 3:1-12 inasema kwamba ulimi ndicho kiungo cha mwili kigumu zaidi kudhibiti. Ukimkubali Mungu audhibiti ulimi wako, Anaweza kutamka sifa kukupitia wewe kwa lugha ambayo haujawahi kuijua. Kunena kwa ndimi, wakati ni tukio halisi kutoka kwa Mungu, ni tendo la kweli la uwasilishaji/unyenyekevu.

**(3) Je unaweza kunena kwa ndimi wakati wowote?**
**Je, unaweza kunena kwa ndimi sasa hivi mbele yangu?**

Pengine njia mwafaka ya kulijibu swali hili ni kulinganisha hali hiyo na uhusiano wako na mwandani wako – au mwenzako katika ndoa. Kuna mazungumzo fulani mnayofanya na huyu mwenzako faraghani. Kunena kwa ndimi ni mazungumzo ya undani na Mungu mwenyewe. Sio jambo la kuonyesha mbele ya watu ili kujilimbikizia sifa.

**15. Jadili Hoja C-6: Hutoa karama za Roho Mtakatifu (Dakika 5-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 35-36)**

Iwapo kuna muda, unaweza kujadili baadhi ya vipaji vya Roho Mtakatifu. Tumia maelezo ya ukurasa 35-36 kwenye Mwongozo wa mwanafunzi kupitia mada hii.

**16. Kuomboleza Roho Mtakatifu (Dakika 5-15)**

Swali la 7 na 8 katika Mwongozo wa somo Zoezi la 5, yanatoa fursa ya kujadili swala la jinsi mafikira na tabia zetu zinaweza kuathiri uhusiano wetu na Roho Mtakatifu. Toa mifano kadhaa ya jinsi tunavyoweza kumuomboleza Roho Mtakatifu kwa matendo yetu na kutoamini kwetu.

4

**Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 5, "Roho Mtakatifu ni nani?"**

Swali 7: Soma Waefeso 4: 29-32. Roho Mtakatifu wa Mungu ana hisia. Hisia zako zaweza kumuathiri. Unapewa ushauri upi kuhusu uhusiano wako na Roho Mtakatifu?

Swali 8: Ni baadhi ya mambo gani Wakristo wanaweza kufanya ambayo yanaweza kumhuzunisha Roho Mtaktifu?

**17. Matumizi binafsi (Dakika 5-10)**

**A. Tathmini uhusiano wangu wa sasa na Roho Mtakatifu.**

Tumia tendo la 3 katika mwongozo wa somo zoezi la 6 kusonga katika sehemu ya matumizi binafsi. Tendo hili linawauliza wanafunzi kutathmini uhusiano wao wa sasa na Roho Mtakatifu katika mambo sita tofauti maishani mwao. Unaweza kuwaagiza wanafunzi waseme majibu yao kwa kila hoja. Ikiwa wanafunzi wako ni wanyamavu, unaweza kuwauliza sehemu hii faraghani, ama katika vikundi vidogo vya watu 2-3.

**Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 6, "Roho Mtakatifu maishani mwangu."**

Tendo la 3: Kwa dakika chache fikiria sehemu aliyonayo Roho Mtakatifu katika maisha yako leo hii. Soma kila kauli zifuatazo na kisha uweke alama kwa kila moja ya chaguzi hizo tatu inayoelezea vyema uhusiano wako wa sasa na Roho Mtakatifu.

| | Mara Nyingi | Wakati mwingine | Nadra |
|---|---|---|---|
| A. Hunihukumu dhidi ya dhambi. | | | |
| B. Hunisaidia kuelewa Biblia. | | | |
| C. Hunisadia kuona tofauti kati ya ukweli na majaribu ya uongo ya Shetani. | | | |
| D. Hunifariji wakati wa shida. | | | |
| E. Hunionyesha mahali napaswa kukua. | | | |
| F. hunisaidia kubadilisha nia yangu kuhusu watu walio na mamlaka juu yangu . | | | |



**B. Ni wapi ninapohitaji usaidizi wa Roho Mtakatifu sasa?**

Angazia matumizi binafsi leo kwa kujifunza jinsi ya kumruhusu Roho Mtakatifu kukusaidia katika shughuli zako za kila siku. Waagize wanafunzi watazame majiibu waliyoyaadika kuhusu swali la 6C kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 6, ambalo linasema, **“Je, kuna hali au shida katika maisha yako leo hii ambapo unahitaji Roho Mtakatifu akusadie ufuate kweli? Fafanua hali hiyo kwa kifupi.”**

Waagize wanafunzi wako kuandika vitu viwili au vitatu wanavyoweza kufanya katika hali fulani na ambavyo vinaweza kuwasaidia kupata ukweli wa Mungu. Wanaweza kuyaandika mawazo yao katika Mwongozo wa somo Zoezi la 6 au katika kijikaratasi tofauti.

> **Kutoka kwa Mwongozo wa somo Zoezi la 6, “Roho Mtakatifu maishani mwangu.”**
>
> Swali la 6C: Je, kuna hali au shida katika maisha yako leo hii ambapo unahitaji Roho Mtakatifu akusadie ufuate kweli? Fafanua hali hiyo kwa kifupi.

**18. Kazi za ziada**

A. Wape mjarabu kuhusu Yohana 16:13 mwishoni mwa darasa.

B. Weka Alama kwa Mwongozo wa somo; mazoezi 4, 5, na 6.

**19. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

# Somo La 5
# Mtihani

**1. Utangulizi**

Fanya utangulizi wa somo litakalofuata.

A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi ifuatayo utakayofundisha.

B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Mpya. Wanapaswa kupata nakala safi ya ***Orodha ya Kazi za Darasani.*** Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.

C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kijacho darasani.

**2. Wape mtihani wa Somo hili.**



**3. Ikiwa bado hujafanya hivyo, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambayo umesahihisha.**

# Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

# Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

# Mtihani

# Majibu ya mtihani

# Cheti cha Somo

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.

**Jina**___________________________ Maisha ya mkristo yenye mafanikio

**Tarehe**_________________________ **Mtihani wa Toleo la 5**

**Darasa**_________________________ ________**Gredi**

## Maswali ya Kweli au Si Kweli (Alama 2 kwa kila swali)

**Maelekezo:** Weka alama ya ___X_____ ikiwa jibu ni kweli.
Weka alama ya ___O_____ ikiwa jibu si kweli.

1.________Mkristo haitaji kukua kiroho.

2.________Mtu anayeishi katika dhambi amekufa kiroho.

3.________Kuwa Mkristo aliyefanikiwa ni lazima ujifunze kudhibiti hisia zako.

4.________Kabla ya kufanya anachopenda Mungu ni lazima ujue anachokuhitaji ufanye.

5.________Mkristo aliyefanikiwa huwa hatendi makosa.

6.________Roho mtakatifu hatendi kitu kwa maisha ya mtu asiye Mkristo.

7.________Wakristo hawapaswi kufanya malengo ya kina kwa sababu Roho Mtakatifu atawasaidia.

8.________Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu ni karama kutoka kwa Mungu kutusaidia kuwa na nguvu zaidi na tuweze kufaulu.

9.________Ukuwa Mkristo, papo kwa hapo Mungu anabadili mtazamo wako, hisia na lengo lako.

10._______Roho Mtakatifu ni jina lingine la Yesu Kristo.

11._______Mungu ananena na watu kupitia dhamiri zao.

12._______Kila mtu huhisi kuwa na hatia anapotenda dhambi.

13._______Wakristo wanapaswa kuwa huru na wazi kuwaambia wengine kuhusu hisia zao.

14._______Njia mwafaka ya kumaliza hisia mbaya katika maisha ya watu ni kuwaambia ukweli. (Waeleze jinsi unahisi.)

### Maswali ya kweli au si kweli

15.______Ni lazima Wakristo kuwa na mtazamo wa kibiblia kama watazieleza hisia zao jinsi Mungu anawahitaji kujieleza.

16.______Unapaswa kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu ili kuwa Mkristo aliyefanikiwa na kuweza kufika mbinguni.

17.______Biblia inasema uko huru kufanya mambo ambayo yanaumiza watu wengine.

18.______Roho Mtakatifu alikufa msalabani kulipia gharama ya dhambi zetu.

### Maswali ya kuchagua kati ya majibu mengi

Chagua jibu sahii na uandike hefuri ya jibu kwenye nafasi iliyochwa. (Alama 2 kwa kila moja)

1._______Roho Mtakatifu ni:

A. Mungu Baba.
B. Yesu.
C. Sawa na Mungu Baba pamoja na Mwana wa Mungu.

2._______Uifahamisha jamii yako kuhusu kile kristo ametenda katika maisha yako, Unapaswa?

A. Kubishana kila wakati.
B. Kubishana kwa wakati fulani.
C. Kuwapinga.

3._______Roho Mtakatifu anataka kuongoza watu katika kweli:

A. Kabla ya wao kuwa wakristo.
B. Baada ya wao kuwa wakristo.
C. Kila wakati.

### Maswali ya kulingana

Jaza herufi sahihi katika nafasi iliyowachwa (Alama 2 kwa kila moja)

| | | | |
|---|---|---|---|
| ____1. | Roho | A. | Kuona |
| ____2. | Utu | B. | Akili |
| ____3. | Utu | C. | Hisia |
| ____4. | Sehemu ya mwili | D. | Kusikia |
| ____5. | Sehemu ya mwili | E. | Imekufa ikiwa mtu mwenyewe sio Mkristo |

## Maswali ya majibu mafupi

1. Je, ni hatua zipi tano unapaswa kuchukua ili kuwa Mkristo aliyefanikiwa? (Alama 10)
   1. ______________________
   2. ______________________
   3. ______________________
   4. ______________________
   5. ______________________

2. Je, Roho Mtakatifu anafanya nini leo? (Alama 6)
   a.______________________
   b.______________________
   c.______________________

3. Katika kozi hii, tulitumia siku moja kuzungumzia jinsi ya kuweka malengo. (Alama 10)
   a. Toa mfano moja wa lengo uliloweka wiki hii.

      ______________________
      ______________________
      ______________________
      ______________________

   b. Kwa kifupi eleza kilichofanyika ulipojaribu kufikia lengo lako.

      ______________________
      ______________________
      ______________________
      ______________________

4. Kwa nini Mkristo anapaswa kuweka malengo? (Alama 5)

   ______________________
   ______________________
   ______________________
   ______________________

5. Andika vifungu vya kukariri hapa chini ama nyuma ya karatasi hii. (Alama 17)

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio
## Mtihani Toleo La 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

**Ukurasa Wa 1**
**Maswali Ya Kweli au Si Kweli**
(Alama 2 kwa kila moja)

1. 0 Si Kweli
2. X Kweli
3. X Kweli
4. X Kweli
5. 0 Si Kweli
6. 0 Si Kweli
7. 0 Si Kweli
8. X Kweli
9. 0 Si Kweli
10. 0 Si Kweli
11. X Kweli
12. 0 Si Kweli
13. 0 Si Kweli
14. 0 Si Kweli

**Ukurasa Wa 2**

15. X Kweli
16. 0 Si Kweli
17. 0 Si Kweli
18. 0 Si Kweli

**Maswali ya kuchagua kati ya majibu mengi**

(Alama 2 kwa kila moja)

1. C
2. C
3. C

**Maswali ya kulingana**

(Alama 2 kwa kila moja)

1. E
2. B ama C
3. B ama C
4. A ama D
5. A ama D

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio
## Mtihani Toleo La 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

**Ukurasa Wa 3**

**Maswali ya majibu mafupi**

1. Alama 10
   1. Kua Mkristo (Alama 2)
   2. Badilisha jinsi unavyofikria (Alama 2)
   3. Weka malengo mapya (Alama 2)
   4. Jifunze jinsi ya kudhibiti hisia zako (Alama 2)
   5. Wafahamishe wengine kile Kristo amefanya katika maisha yako (Alama 2)

2. Alama 6 *Majibu ya kupendekezwa*:

   -- Anatufunza

   -- Anatuelekeza kwa kweli

   -- Anazalisha matunda ya Roho Mtakatifu ndani ya maisha yetu

   -- Anatupatia Ubatizo wa Roho Mtakatifu

   -- Anatupatia zawadi zengine

3. A. *Jibu Binafsi* (Alama 5)

   B. *Jibu Binafsi* (Alama 5)

4. Alama 5

   *Majibu ya kupendekezwa*

   Para poder hacer la voluntad de Dios. (Lo que Dios quiere que hagamos.)

**Ukurasa Wa 4**

5. Alama 17

   1 Wakorintho 10:29

   Yohana 16:13

**Hongera**

________________________________________

Amemaliza

# Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio
utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi __________________________

Tarehe ______________________________

**Hongera**

________________________________________

Amemaliza

Maisha ya Kikristo yenye mafanikio

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio
utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi __________________________

Tarehe ______________________________